BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA WA MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A (GATCE) 2018

## 612 URAIA

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A 2018

# 612 URAIA

*Kimechapishwa na:*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2018**

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO

DIBAJI ........ iv
1.0 UTANGULIZI ........ 1
2.0 TATHMINI KWA KILA SWALI. ........ 2
2.1 SEHEMU A: ........ 2
2.1.1 Swali la 1 ........ 2
2.1.2 Swali la 2 ........ 4
2.1.3 Swali la 3 ........ 6
2.1.4 Swali la 4 ........ 9
2.1.5 Swali la 5 ........ 11
2.1.6 Swali la 6 ........ 14
2.1.7 Swali la 7 ........ 16
2.1.8 Swali la 8: ........ 18
2.1.9 Swali la 9 ........ 20
2.1.10 Swali la 10 ........ 22
2.2 SEHEMU B ........ 24
2.2.1 Swali la 11 ........ 24
2.2.2 Swali la 12 ........ 29
2.2.3 Swali la 13 ........ 34
2.3 SEHEMU C ........ 40
2.3.1 Swali la 14 ........ 40
2.3.2 Swali 1a 15 ........ 43
2.3.3 Swali la 16 ........ 48
3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU CHA WATAHINIWA KWA MADA ........ 52
4.0 HITIMISHO: ........ 52
5.0 MAPENDEKEZO ........ 53
Kiambatisho ........ 55

# DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania linayo furaha kutoa taarifa ya watahini kuhusu ufaulu wa watahiniwa wa Mtihani wa Kuhitimu Ualimu Daraja la Tatu A kwa somo la Uraia. Taarifa hii imeandaliwa ili kutoa mrejesho wa ufaulu katika mitihani kwa wanachuo, wakufunzi, waandaaji sera na wadau wa elimu kwa ujumla.

Taarifa hii ni tathmini ya mwisho ambayo pamoja na mambo mengine, inaonesha mafanikio katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Uraia. Kimsingi majibu ya watahiniwa ni uthibitisho wa kipi mfumo wa elimu uliweza au ulishindwa kuwapa watahiniwa wawapo katika mafunzo ya Ualimu katika daraja hili.

Uchambuzi uliowasilishwa katika taarifa hii una lengo la kuchangia katika kuelewa zaidi sababu za watahiniwa kufanya vibaya au vizuri katika mtihani wao. Mrejesho huu utawawezesha viongozi wa elimu, viongozi wa vyuo, wakufunzi na wanavyuo kupata mbinu muafaka katika kuboresha ufaulu wa watahiniwa katika mitihani ijayo inayoandaliwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.

Baraza la Mitihani la Tanzania litapenda kupokea maoni na mapendekezo kutoka kwa wakufunzi, wanavyuo na umma kwa ujumla ambayo yatatumika katika kuboresha taarifa za uchambuzi wa majibu ya watahiniwa zitakazofuata.

Mwisho Baraza linapenda kuwashukuru Maafisa Mitihani, Watahini wa masomo na Walimu wa masomo na wadau wote waliohusika katika uchambuzi wa takwimu na kutayarisha taarifa hii.

Dkt. Charles E. Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Mtihani wa somo la Uraia kwa watahiniwa wa Ualimu ngazi ya Astashahada ulifanyika mwezi Mei, 2018 na uliandaliwa kwa kuzingatia muhtasari wa somo la Uraia wa mwaka 2009.

Mtihani wa **612 Uraia** uligawanyika katika sehemu **A**, **B** na **C**. Sehemu A, ilikuwa na maswali kumi (10) ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote, kila swali lilikuwa na alama nne (04). Sehemu B na C zilikuwa na maswali matatu (03) kila moja, ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali mawili tu kwa kila sehemu. Sehemu B na C zilikuwa na alama (30) kila moja. Hivyo mtihani ulikuwa na maswali kumi na sita (16) na mtahiniwa alitakiwa kujibu jumla ya maswali kumi na nne (14).

Ufaulu kwa watahiniwa katika mtihani wa 612 Uraia kwa mwaka 2018 ulikuwa wa kiwango kizuri ambapo asilimia **99.98** ya watahiniwa wote waliofanya mtihani walipata wastani wa alama 40 na zaidi. Ufaulu huu umegawanyika katika viwango vitatu vya ufaulu ambavyo ni 'vizuri', 'wastani', na 'hafifu'. Ufaulu kwa kiwango kizuri unaanzia alama 70 hadi 100; kiwango cha wastani alama 40 hadi 69; na kiwango hafifu alama 00 hadi 39. Aidha, chati za viwango vya ufaulu zimeambatishwa ili kufafanua ufaulu kwa watahiniwa ambapo rangi ya kijani inawakilisha ufaulu kwa kiwango kizuri, rangi ya njano inawakilisha ufaulu wa kiwango cha wastani na rangi nyekundu inawakilisha ufaulu wa kiwango hafifu.

Taarifa hii inachambua maswali yaliyojibiwa vizuri, kwa wastani na hafifu ili kukuza kiwango cha ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Uraia. Uchambuzi huu unalenga kuonesha jinsi watahiniwa walivyojibu maswali katika mtihani wa 612 Uraia. Sampuli za majibu yao zimeambatishwa ili kuonesha kilichotarajiwa kufanywa na watahiniwa. Aidha, taarifa inaonesha pia sababu zilizowafanya watahiniwa wachache kutopata alama za juu katika majibu ya maswali katika baadhi ya mada. Hivyo, uchambuzi huu umeweka mpango mkakati wa kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Uraia kwa mada hizo ili kuboresha ufaulu kwa watahiniwa katika mitihani yote inayosimamiwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.

## 2.0 TATHMINI KWA KILA SWALI


Mtihani wa Uraia (612) uligawanyika katika sehemu A, B na C. Sehemu A ya mtihani ilikuwa na jumla ya maswali 10 yaliyotoka katika mada za *Taaluma* na *Utaalamu* (Ufundishaji) na mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote. Sehemu B na C ilikuwa na maswali matatu kila moja, yaliyotoka katika mada za *Taaluma* na *Ufundishaji* mtawalia ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali mawili kwa kila sehemu.

## 2.1 SEHEMU A

Sehemu A ilikuwa na maswali kumi (10) ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu yote. Kila swali lilikuwa na alama nne (04). Hivyo sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama arobaini (40).

### 2.1.1 Swali la 1

Swali hili lilitoka katika mada ya *"*Dola" katika kipengele cha Mahakama. Swali lilimtaka mtahiniwa aorodheshe kazi nne za Mahakama Kuu ya Tanzania. Kati ya watahiniwa 5086 waliofanya swali hili, watahiniwa 4919, sawa na asilimia 96.7, walipata alama 03 hadi 04 ambao ni ufaulu mzuri kwa swali hili. Watahiniwa 129, sawa na asilimia 2.6, walikuwa na ufaulu wa wastani wa alama 02 hadi 2.5, na watahiniwa 38, sawa na asilimia 0.7 walipata alama 00 hadi 1.5, ambao ni ufaulu hafifu. Chati Na. 1 inaonesha viwango vya ufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.





**Chati Na. 1:** Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia

Watahiniwa wengi (96.7%) waliopata alama kati ya 03 hadi 04 walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada husika. Watahiniwa hao walielewa matakwa ya swali na hivyo kuweza kutoa majibu sahihi ya swali hili. Mfano wa majibu hayo ni*: Kusikiliza makosa ya jinai, kushughulikia*

*makosa/kesi za kikatiba, kushughulikia kesi au malalamiko yanayotokana na uchaguzi* na *kushughulikia rufaa kutoka Mahakama za wilaya na mahakama za Hakimu mkazi*. Kielelezo 1.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili kwa usahihi.

**Kielelezo 1.1**


1. Kazi za Mahakama Kuu ya Tanzania ni
(i) Kutatua migogoro ya wananchi. Mahakama Kuu huweza kutatua migogoro kwa kutafuta suluhisho la malalamiko mbalimbali
(ii) Kutoa kibali cha ukataji wa rufaa kwenda katika mahakama ya rufaa. mahakama ya rufaa ndio ngazi ya mwisho ya mahakama. Hivyo ikiwa mlalamikaji hakuridhika ~~na~~ maamuzi ya mahakama kuu, mahakama hii humpa rufaa
(iii) Kusimamia kanuni na sheria za nchi. Mahakama kuu inaowajibu wa kuhakikikisha sheria na kanuni za nchi zinatunzwa
(iv) Kulinda na kutetea haki za binadamu. Mahakama kuu pia hutetea na kulinda haki za binadamu kwa kutatua migogoro bila ya kufungamana na upande wa mlalamikaji au mlalamikiwa


Kielelezo 1:1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri kwa kuorodhesha kazi nne za Mahakama Kuu ya Tanzania.

Aidha, wapo watahiniwa (2.6%) walioweza kutaja baadhi ya kazi za Mahakama Kuu ya Tanzania, hivyo walipata alama za wastani. Wengine kati yao walitaja hoja sahihi na zisizo sahihi na wengine walirudia hoja zaidi ya mara moja. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alichanganya kazi mbili za mahakama na mbili za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hivyo kupata alama pungufu.

Aidha, asilimia 0.7 ya watahiniwa waliopata alama hafifu katika swali hili, walionesha kutoelewa matakwa ya swali na wengine kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika. Kwa mfano, mtahiniwa aliandika baadhi ya mada ndogo zilizopo kwenye muhtasari wa somo la Uraia katika ngazi ya

Astashahada ya Ualimu badala ya kazi za Mahakama Kuu ya Tanzania kama inavyoonekana katika Kielelezo 1.2.


**Kielelezo 1.2**


(1) Kukuza ujuzi na stadi za Uraia
(2) Uchambuzi wa mada ya mafuala ya Chanya na hasi ya kiserikali na siasa.
(3) Kuyenga dhana tata ya kufundishia ya somo la Uraia.
(4) Mada/maudhui ya somo za Uraia kuwa na uhusiano na Katiba ya Jamuhuri wa muungano wa Tanzania.

Kielelezo 1.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kutoa majibu sahihi katika swali hili ambapo alitakiwa kujibu kwa kuorodhesha hoja kama; kusikiliza makosa ya jinai, kushughulikia makosa/kesi za kikatiba na kushughulikia kesi au malalamiko yanayotokana na uchaguzi.

### 2.1.2 Swali la 2


Swali hili lilitoka katika mada ya "Misingi ya Ufundishaji wa Somo la Uraia". Swali lilimtaka mtahiniwa ataje misingi minne ya ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Uraia. Kati ya watahiniwa 5086 waliofanya swali hili, watahiniwa 2414 sawa na asilimia 47.5 walifanya vizuri kwani waliweza kupata alama 03 hadi 04, watahiniwa 539 sawa na asilimia 10.6 walikuwa na ufaulu wa kiwango cha wastani kwa kupata alama 02 hadi 2.5 na watahiniwa 2133 sawa na asilimia 41.9, walikuwa na ufaulu hafifu kwa kupata alama 00 hadi 1.5 kama inavyoonekana katika Chati Na. 2.




**Chati Na. 2:** *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia*

Watahiniwa waliopata alama 03 had 04 waliweza kutaja misingi ya ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Uraia kama vile: *Msingi unaozingatia masuala mtambuko, msingi unaozingatia urali wa jinsia, msingi unaozingatia matumizi bora ya zana za kufundishia na kujifunzia* na *msingi unaozingatia udadisi kwa wanafunzi*. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika na walielewa matakwa ya swali. Kielelezo 2.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili kwa usahihi.

**Kielelezo 2.1.**



2. i) Msingi unaozingatia masuala mtambuko
(ii) Msingi unaozingatia urali wa jinsia
(iii) Msingi unaozingatia matumizi bora ya zana za kufundishia na kujifunzia
(iv) Msingi unaozingatia udadisi kwa wanafunzi

Kielelezo 2.1. ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kutaja misingi minne ya ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Uraia kulingana na matakwa ya swali.

Aidha, watahiniwa (10.6%) waliokuwa na ufaulu wa wastani walitaja hoja pungufu na kurudia hoja zaidi ya mara moja, wengine walikuwa wakichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliopata alama 00 hadi 1.5 walishindwa kutaja misingi ya ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Uraia. Watahiniwa hao walionesha kutokuwa na maarifa na wengine walishindwa kuelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa alitoa hoja kama vile: *Kutambua uraia, mila na desturi, maadili mema* na *utendaji kazi* ambayo ni masuala mbalimbali yanayofundishwa katika mada za somo la Uraia badala ya kutaja misingi minne ya ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Uraia. Kielelezo 2.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.

**Kielelezo 2.2**



2. i) Ufundishaji na ujifunzaji wa somo la uraia Unaozingatia mwanafunzi kutambua uraia wake.
ii) Ufundishaji na Ujifunzaji Unaozingatia mila, desturi na Utamaduni.
iii) Ufundishaji na ujifunzaji wa somo la uraia Unaozingatia maadili mema kwa mwanafunzi.
iv) Ufundishaji na ujifunzaji wa somo la uraia Unaozingatia utendaji kazi.

Kielelezo 2.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa ambaye alishindwa kukidhi matakwa ya swali ambapo alitakiwa kutaja hoja kama; mantiki katika ufundishaji, ufundishaji na ujifunzaji unaozingatia usawa wa jinsia na kuzingatia ujuzi na stadi katika ufundishaji.

### 2.1.3 Swali la 3

Swali hili lilitoka katika mada ya "Uchambuzi wa Maandiko/Machapisho Muhimu ya Kufundishia na Kujifunzia Somo la Uraia". Mtahiniwa alitakiwa aeleze kwa kifupi umuhimu wa kutumia kiongozi cha mwalimu katika ufundishaji wa somo la Uraia kwa kutoa hoja nne. Watahiniwa 4999, sawa na asilimia 98.3 ya watahiniwa wote waliofanya swali hili walipata


ufaulu mzuri wa alama 03 hadi 04, asilimia 0.7 walipata alama 02 hadi 2.5, ambao ni ufaulu wa wastani, na asilimia 1.0 walipata alama 00 hadi 1.5 ambao ni ufaulu hafifu kama inavyoonekana katika Chati Na. 3.




**Chati Na. 3:** *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia*

Asilimia 98.3 ya watahiniwa waliofanya vizuri swali hili waliweza kueleza kwa kifupi umuhimu wa kiongozi cha mwalimu kama vile: *Humsaidia mwalimu kujua uelekeo wa kile anachofundisha*, *humsaidia kuwaongoza wanafunzi kwa usahihi*, *humsaidia mwalimu kufanya upimaji* na *humsaidia kufikia malengo aliyokusudia*. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika na waliweza kukidhi matakwa ya swali kwa kueleza hoja tatu hadi nne. Kielelezo 3.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili kwa usahihi.

**Kielelezo 3.1**



3. i) Humsaidia mwalimu kujua uelekeo wa kile kitu anachokifundisha
ii) Humsaidia kuwaongoza wanafunzi kwa wahihi
iii) Humsaidia kumrahisishia kazi ya ufundishaji hususa ni katika upimaji wa wanafunzi.
iv) Humsaidia kufikia malengo aliyoyakusudia kwa siku hiyo.

Kielelezo 3.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kueleza umuhimu wa kutumia kiongozi cha mwalimu katika ufundishaji wa somo la Uraia.

Kwa upande mwingine, watahiniwa wachache (0.7%) waliopata ufaulu wa wastani, walishindwa kukidhi idadi ya hoja zilizohitajika na wengine walirudia hoja zaidi ya mara moja. Aidha, wapo waliochanganya hoja sahihi na zisizo sahihi katika majibu yao. Kwa mfano mtahiniwa baada ya kutaja hoja sahihi mbili alichanganya na umuhimu wa kutumia nukuu za somo kwa mwalimu ambayo hayakuwa majibu sahihi.

Watahiniwa walioshindwa swali hili kwa kupata ufaulu hafifu walishindwa kueleza kwa kifupi umuhimu wa kutumia kiongozi cha mwalimu katika ufundishaji. Baadhi yao hawakuelewa kabisa matakwa ya swali. Kwa mfano mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama vile *kiongozi cha mwalimu kumwongoza mwalimu kutekeleza wajibu na majukumu yake kwa wanafunzi, jamii na taifa* majibu ambayo hayakuwa sahihi. Kielelezo 3.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa swali hili.


**Kielelezo 3.2**


3. Umuhimu wa Kiongozi cha mwalimu Ni kumwongoza mwalimu katika kutekeleza wajibu na Majukumu yake kwa wanafunzi, jamii na taifa.

Kielezo 3.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali hili kwa kutoa maelezo ambayo hayakuwa na uhusiano na matakwa ya swali na hivyo kupata alama hafifu.

### 2.1.4 Swali la 4

Swali lilitoka katika mada ya "Utamaduni Wetu". Swali lilikiwa na vipengele viwili. Kipengele (a) kilimtaka mtahiniwa kueleza maana ya maadili, na kipengele (b) kilimtaka mtahiniwa kuainisha mbinu tatu za kurekebisha mmomonyoko wa maadili katika jamii. Watahiniwa 4939, sawa na asilimia 97.1 walikuwa na ufaulu mzuri wa alama 03 hadi 04, watahiniwa 97 sawa na asilimia 1.9 walikuwa na ufaulu wa wastani wa alama 02 hadi 2.5, na watahiniwa 50 sawa na asilimia 01, walipata ufaulu hafifu wa alama 00 hadi 1.5 kama inavyoonekana katika Chati Na. 4.




**Chati Na. 4:** *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia*

Watahiniwa wengi (97.1%) waliopata ufaulu mzuri katika swali hili walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada hii, hali ambayo huenda ilisababishwa na kuwa mada hii inalenga maisha ya kila siku katika jamii na suala la mmomonyoko wa maadili lina mifano dhahiri kutoka katika jamii na mazingira wanamoishi. Aidha, pengine kwa kuwa mada ya maadili hujadiliwa na vyombo mbalimbali vya habari hivyo kufanya watahiniwa kuwa na uelewa mzuri wa mada hii. Baadhi ya majibu yaliyotolewa na watahiniwa hawa kwa kipengele (a) ni kama vile *Maadili ni mienendo na tabia nzuri anazokuwa nazo mtu na zinaendana na kukubalika na jamii,* na katika kipengele (b) baadhi ya mbinu zilizobainishwa ni kama vile *kuwapatia elimu, kutungwa kwa sheria kali kwa watu wote wanaovunja sheria* na *adhabu kali kwa wenye tabia mbaya.* Kielelezo 4.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili kwa usahihi kwa kueleza maana ya maadili na mbinu za kurekebisha mmomonyoko wa maadili katika jamii.

**Kielelezo 4.1**

| | |
|---|---|
| 1. | (a) Maadili ni Mienendo na tabia nzuri anazokuwa |
| | nazo mtu na zinazoendana na kukubalik |
| | a na jamii husika. Mfano heshima kwa |
| | Wakubwa na wadogo, utii |
| | |
| | (b) i/ kukaa na jamii na kueleza au kuwapatia |
| | elimu juu ya kuishi katika jamii |
| | ii/ kutungwa kwa sheria kali kwa watu wote |
| | wanaovunja sheria na kumomonyoko wa |
| | adili |
| | iii/ Adhabu kali kwa wenye Tabia mbaya |
| | wote. |


Kielelezo 4.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili kwa usahihi kwa kueleza maana ya maadili na mbinu za kurekebisha mmomonyoko wa maadili katika jamii.

Hata hivyo, watahiniwa (1.9%) walipata ufaulu wa wastani katika swali hili kwa sababu ya mapungufu mbalimbali katika majibu yao, baadhi yao

walijibu kipengele (a) na kushindwa kipengele (b), wengine walitoa maelezo yasiyo sahihi kwa vipengele vyote, kurudia hoja hasa kipengele (b) na baadhi yao kushindwa kutoa maelezo sahihi ya mbinu za kurekebisha mmonyoko wa maadili katika jamii.

Aidha, watahiniwa wachache (01%) kati ya watahiniwa waliofanya swali hili hawakujibu kwa usahihi na hivyo kupata alama hafifu. Baadhi yao walichanganya maarifa na wengine walionekana kukosa maarifa ya kutosha kuhusu neno maadili na mbinu za kurekebisha mmomonyoko wa maadili katika jamii. Kielelezo 4.2 ni sampuli ya mtahiniwa aliyeshindwa kueleza maana ya maadili na mbinu za kurekebisha mmomonyoko wa maadili.

**Kielelezo 4.2**


4 a) Maadili ⇒ Ni hali ya mtu kupata malezi ambayo yatamjenga kiakili, kimwili na kiroho


b/ i/ Mbinu ya kumualika mtaalamu
ii/ Mbinu ya Maswali na Majibu
iii/ Onyesho Mbinu

Kielelezo 4.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kutoa maana ya maadili kwa usahihi na kuonesha mbinu za kufundishia badala ya mbinu za kurekebisha mmomonyoko wa maadili kwenye kipengele (b), kinyume na mahitaji ya swali.

### 2.1.5 Swali la 5

Swali hili lilitoka katika mada ya "Zana za Kufundishia na Kujifunzia Uraia". Swali lilimtaka mtahiniwa kuorodhesha faida nne za kutunza zana za kufundishia na kujifunzia somo la Uraia. Miongoni mwa watahiniwa hao, watahiniwa 4990, sawa na asilimia 98.1 walijibu vizuri swali na kupata alama 03 hadi 04. Watahiniwa 36, sawa na asilimia 0.7


waliorodhesha hoja pungufu na hivyo kupata alama za wastani ambazo ni alama 02 hadi 2.5 na asilimia 1.2 ya watahiniwa walipata ufaulu hafifu wa alama 00 hadi 1.5, kama inavyoonekana katika Chati Na. 5.




**Chati Na. 5:** *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia*

Watahiniwa walio wengi (98.1%) waliofanya swali hili walipata ufaulu mzuri kwani walionesha uwezo wa kuhawilisha maarifa kwa sababu mada hii hufundishwa kwenye masomo mengi ambayo yapo kwenye mtaala wa mafunzo yao. Watahiniwa hao pia walionesha kuelewa matakwa ya swali na hivyo kuweza kutoa majibu sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa aliorodhesha faida sahihi za kutunza zana kama vile: *Kuepusha gharama ya kununua mara kwa mara*, *kuepusha hatari zinazoweza kusababishwa na kuzagaa kwa zana*, *kwa matumizi ya baadae* na *kuwa na hazina kubwa ya zana* kama inavyoonekana katika Kielelezo 5.1.

**Kielelezo 5.1**



5. Faida nne za kutuma zana za kufundishia
(i) Kuepusha gharama ya kununua mara kwa mara
(ii) Kuepusha hatari zinazoweza kusababishwa na kuzagaa kwa zana.
(iii) Kutumia kwa matumizi ya baadaye
(iv) Kuwa na hazina kubwa ya zana za kufundishia na kujifunzia.

Kielelezo 5.1 ni sampuli ya mtahiniwa aliyejibu vizuri kwa kuorodhesha faida nne za kutunza zana za kufundishia na kujifunzia somo la Uraia.

Aidha, baadhi ya watahiniwa wachache (0.7%) waliopata alama za wastani, walichanganya vipengele sahihi na visivyo sahihi na wengine walitaja hoja pungufu na hivyo kupata alama pungufu.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliopata alama 00 hadi 1.5 walishindwa kutoa majibu yaliyokidhi matakwa ya swali. Baadhi yao walichanganya maarifa na kuorodhesha faida za zana za kufundishia na kujifunzia badala ya faida za kutunza zana za kufundishia na kujifunzia. Kwa mfano, mtahiniwa aliorodhesha hoja kama vile: *Husaidia kujenga dhana kwa urahisi, kukuza udadisi na ubunifu, kuchochea ari ya kulipenda somo* na *kuleta ukweli wa somo.* Kielelezo 5.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kuorodhesha faida za kutunza zana za kufundishia na kujifunzia somo la Uraia.

**Kielezo 5.2**



5. Ufuatao ni faida za kutumia
zana za kufundishia na kujifunzia.
Husaidia kujenga dhana kwa urahisi
Sababu zana huendana na malengo
mahususi ya ~~eh~~ somo la uraia.
Kukuza udadisi na ubunifu.
Mwanafunzi hukuza maarifa na
stadi kwa udadisi na ubunifu kupitia
zana ya kufundishia na kujifunzia.
Kuchochea ari ya kupenda somo
Mwanafunzi anapojifunza kwa
vitu vielelezi hufurahia na kusaidia
kukuza ari ya kupenda somo.
Huleta ukweli wa somo. Zana
huendana na malengo mahususi
ya somo hivyo mwanafunzi huele
wa kwa undani zaidi kupitia zana.

Kielelezo 5.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyechanganya maarifa, mtahiniwa alielezea faida za kutumia zana badala ya faida za kutunza zana.

### 2.1.6 Swali la 6

Swali hili lilitoka katika mada ya "Uchumi wa Tanzania", ambapo lilimtaka mtahiniwa kwa kutumia hoja nne aoneshe faida za mipango katika uchumi. Miongoni mwa watahiniwa waliofanya swali hili, watahiniwa 4220, sawa na asilimia 83 walipata ufaulu mzuri wa alama 03 hadi 04, watahiniwa 332, sawa na asilimia 6.5, walipata ufaulu wa wastani wa alama 02 hadi 2.5, na watahiniwa 534 sawa na asilimia 10.5, walipata alama 00 hadi 1.5 ambao ni ufaulu hafifu. Chati Na. 6 inaonesha viwango vya ufaulu katika swali hili.


.




**Chati Na. 6:** *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia*

Asilimia 83 ya watahiniwa waliopata alama 03 hadi 04 waliweza kukidhi matakwa ya swali kwa kuonesha faida za mipango katika uchumi kama swali lilivyohitaji. Ufaulu huo pengine ulisababishwa na upana wa suala la mipango katika uchumi kwani halitegemei kufundishwa darasani tu. Pia yawezekana walijisomea vitabu na rejea mbalimbali na pia waliweza kupata maarifa yanayohusu mipango kwenye vyombo vya habari. Kwa mfano, mtahiniwa alionesha faida za mipango katika uchumi kama vile: *Kukuza uchumi, kuboresha miundo mbinu, kupata maendeleo endelevu* na *kuboresha huduma katika jamii*. Kielelezo 6.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri.

**Kielelezo 6.1**



6 Faida za mipango katika uchumi.
(i) Kukuza uchumi.
(ii) Kuboresha miundombinu.
(iii) Kupata maendeleo endelevu.
(iv) Kuboresha huduma mbalimbali katika jamii.

Kielelezo 6.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa ambaye aliweza kuonesha faida nne za mipango katika uchumi.

Aidha, watahiniwa waliopata alama 02 hadi 2.5 walionesha udhaifu wa namna mbalimbali katika majibu yao. Baadhi yao walichanganya hoja sahihi na zisizosahihi wakati wengine walitaja hoja pungufu na hivyo kupata alama za wastani.

Hata hivyo, watahiniwa waliopata alama kati ya 00 hadi 1.5 walishindwa kutaja faida za mipango kama swali lilivyoelekeza. Baadhi yao walionesha kutokuwa na maarifa kabisa katika mada husika wakati wengine walichanganya maarifa. Kwa mfano, yupo mtahiniwa ambaye alionesha faida za kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi badala ya kutaja faida za mipango katika uchumi, kama vile *kuweka hali ya maisha kuwa bora*, *kuendeleza pato la taifa*, *kuendeleza maendeleo ya familia na jamii* na *kupunguza hali ya tegemezi* kama inavyooneka katika kielelezo 6.2.


**Kielelezo 6.2.**


6. Faida za Mipango katika uchumi
i) Kuweka hali ya Maisha Kuwa bora
ii) Kuendeleza pato la nchi
iii) Kuendeleza Maendeleo ya familia na Jamii
iv) kupunguza hali ya tegemezi

Kielelezo 6.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kuonesha faida za mipango katika uchumi badala yake alionesha faida za kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi.

### 2.1.7 Swali la 7

Swali hili lilitoka katika Mada ya "Maandalizi ya Kufundisha Somo la Uraia". Swali lilimtaka mtahiniwa atoe maana ya istilahi (a) ujuzi mpya na (b) Tafakuri, kama zinavyotumika katika andalio la somo la Uraia. Kati ya watahiniwa wote waliofanya swali hili, watahiniwa 3047 sawa na asilimia 59.9 walipata ufaulu mzuri wa alama 03 hadi 04, watahiniwa 1975 sawa na asilimia 38.8 walipata ufaulu wa wastani wa alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 64 sawa na asilimia 1.3 walipata ufaulu hafifu wa alama 00 hadi 1.5 kama inavyoonekana katika Chati Na. 7.





**Chati Na. 7:** *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia*

Watahiniwa 59.9% waliopata ufaulu mzuri waliweza kueleza maana sahihi za istilahi zote mbili zilizoulizwa. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika kwani mada hiyo hufundishwa karibu katika masomo yote ya ufundishaji. Majibu sahihi katika istilahi hizo yalikuwa kama ifuatavyo:

> (a) Ujuzi mpya ni hatua ambayo mwalimu anatakiwa kufikiri kwa kina kuhusu stadi na maarifa atakayotumia mwanafunzi kujenga ujuzi unaotarajiwa na (b) Tafakuri ni hatua inayomtaka mwalimu kuwaongoza wanafunzi kutafakari jinsi maarifa waliyojifunza yanavyohusiana na maisha yao na ujuzi wanaotarajiwa kuupata.

Kielelezo 7 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri.

**Kielelezo 7**


7 Maana ya istilahi zifuatazo
a) Ujuzi mpya - Hii ni hatua ya pili katika mchakato mzima wa Ufundishaji na Ujifunzaji ambapo mwalimu huweza kutoa Maudhui ya Mada Mpya kwa wanafunzi na kuweza kulitolea Ufafanuzi zaidi.

b) Tafakuri - Hii ni hatua ya nne katika tendo nzima la Ufundishaji na Ujifunzaji ambapo Mwalimu huweza kulihusianisha Mada aliyofundisha na Mazingira ya kawaida ya Mwanafunzi katika tendo nzima la Ufundishaji na Ujifunzaji.


Kielelezo 7 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kueleza maana ya istilahi "ujuzi mpya" na "tafakuri" kama zinavyotumika katika andalio la somo.

Aidha, baadhi ya watahiniwa waliopata ufaulu wa wastani kwa kupata alama 02 hadi 2.5 walishindwa kueleza moja ya kipengele kwa usahihi na wengine walishindwa kabisa kueleza kipengele cha pili.

Aidha, watahiniwa wachache (1.3%) waliopata alama 00 hadi 1.5 walishindwa kutoa maana ya istilahi zilizoulizwa. Baadhi yao walionekana kukosa maarifa ya kutosha katika mada husika na wengine walichanganya maarifa. Baadhi ya watahiniwa walitoa maana ya hitimisho kwenye andalio la somo badala ya tafakuri na wengine walichanganya na kitendo cha mwalimu kutoa kazi (mazoezi) kwa wanafunzi.

### 2.1.8 Swali la 8:


Swali hili lilitoka katika mada ya "Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji Somo la Uraia". Swali lilimtaka mtahiniwa abainishe stadi nne muhimu zinazohitajika kwa mtu kuwa raia mwema wa Tanzania. Watahiniwa 3546, sawa na asilimia 69.7 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata ufaulu mzuri wa alama 03 hadi 04. Watahiniwa 730 sawa na asilimia 14.4 walipata ufaulu wa wastani wa alama 1.5 hadi 02, na watahiniwa 810 sawa na asilimia 15.9 walikuwa na ufaulu hafifu wa alama 00 hadi 1.5. Viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa kifupi vimeoneshwa katika Chati Na. 8 kama ifuatavyo:




**Chati Na. 8:** *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia*

Watahiniwa waliopata ufaulu mzuri katika swali hili waliweza kubainisha stadi zinazohitajika kwa mtu kuwa raia mwema wa Tanzania kwa ufasaha. Watahaniwa hao waliweza kubaini matakwa ya swali na walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada hii. Waliweza kutoa majibu sahihi kama vile: *Stadi za mawasiliano*, *stadi za kufanya maamuzi sahihi*, *stadi za kushiriki na kushirikiana* na *stadi za kufikiri kwa kina*. Kielelezo 8.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kubainisha stadi muhimu zinazohitajika kwa mtu kuwa raia mwema wa Tanzania.

**Kielelezo 8.1.**


8. (i) Uwajibikaji
Mtu anayetakiwa kuwa raia mwema wa ~~wa~~ Tanzania ni yule anayewajibika katika majukumu mbalimbali.
(ii) Ushirikiano
Raia mwema wa nchi ya Tanzania anatakiwa kuwa na ushirikiano na wenzake katika nyanja mbalimbali.
(iii) Kushiriki kutoa maamuzi yenye busara yanayolenga kuendeleza nchi sio yanayodidimiza nchi.
(iv) Mawasiliano
Raia mwema wa nchi ya Tanzania anatakiwa kuwa na mawasiliano mema baina yake na wenzake au viongozi wa nchi yake.


Kielelezo 8.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kubainisha stadi nne muhimu zinazohitajika kwa mtu kuwa raia mwema wa Tanzania.

Asilimia 14.4 ya watahiniwa walipata alama 02 hadi 2.5, wengi wao walitaja hoja pungufu na wengine kurudia hoja zaidi ya mara moja. Aidha katika kundi hili wapo waliochanganya hoja sahihi na zisizo sahihi.

Aidha, asilimia 15.9 ya watahiniwa walikuwa na ufaulu hafifu, wengi wao walikosa maarifa ya kutosha katika mada husika na wengine walishindwa kubainisha matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa alionesha taratibu za kuzingatiwa kwa mtu anayetaka kuomba uraia wa nchi fulani kwa kutoa hoja kama *kujaza fomu ya uraia*, *kutangazwa kwa jina lake*, *kuukana utaifa*

*wa nchi aliyotoka* na *kutokuwa na makosa ya jinai* badala ya kubainisha stadi muhimu zinazohitajika kwa mtu kuwa raia mwema wa Tanzania kama kama inavyoonekana katika kielelezo 8.2.


**Kielelezo 8.2**


8. i) Kujaza fomu ya uraia.
ii) Kutangazwa kwa jina lake.
iii) Kuukana utaifa wa nchi aliyotoka.
iv) Kutokuwa na makosa ya jinai.

Kielelezo 8.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali kwa kubainisha sifa za mtu kupata uraia wa Tanzania.

### 2.1.9 Swali la 9


Swali hili lilitoka katika mada ya "Upimaji na Tathmini". Swali lilimtaka mtahiniwa kuchambua zana mbili za upimaji katika somo la Uraia. Watahiniwa 4580, sawa na asilimia 90.1 ya watahiniwa walifanya swali vizuri kwa kupata alama 03 hadi 04. Watahiniwa 373 sawa na asilimia 7.3 walipata ufaulu wa wastani wa alama 02 hadi 2 na watahiniwa 133 sawa na asilimia 2.6 walipata ufaulu hafifu kwa kupata alama 00 hadi 1.5 kama inavyoonesha katika Chati Na. 9.




**Chati Na. 9:** *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia*

Watahiniwa waliopata ufaulu mzuri katika swali hili walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha katika dhana ya upimaji na walielewa matakwa ya swali. Kwa mfano, baadhi yao waliweza kuchambua zana za upimaji katika somo la Uraia kwa kutoa hoja kama vile *mitihani*, *mazoezi na majaribio* kama inavyoonekana katika kielelezo 9.1.

**Kielelezo 9.1**


9. Kuchambua zana mbili za upimaji kati ka somo la ~~urai~~ uraia.

(i) Mitihani
Hizi ni zana za upimaji amba zo tutumika kupima mwanafunzi baada ya kumaliza mada za Somo la Uraia.


(ii) Mazoezi na Majaribio
Ni zana zinazo tumika kupima mwanafunzi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

Kielelezo 9.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kuchambua kwa ufupi zana za upimaji katika somo la Uraia vizuri kulingana na matakwa ya swali.

Watahiniwa waliopata ufaulu wa wastani walikuwa na mapungufu mbalimbali katika majibu yao. Mapungufu hayo ni kama kushindwa kutoa maelezo sahihi ya hoja zao, kuchanganya hoja sahihi na zisizo sahihi pamoja na kutoa hoja pungufu.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliopata ufaulu hafifu katika swali hili, walikosa maarifa kabisa katika mada husika na wengine walichanganya maarifa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alichanganya maarifa kwa kuonesha maana ya zana za kufundishia na kujifunzia na mwingine alionesha aina za upimaji kama vile *upimaji endelevu* na *upimaji tamati*. Kielelezo 9.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali


**Kielelezo 9.2**


9 (i) Zana za Ufundishaji:
=> Hizi ni zana anazotumia mwalimu kufundishia somo.
mfano: Chaki, Kitabu cha mwalimu.
(ii) Zana za kujifunzia:
=> Hizi ni zana anazotumia mwanafunzi kujifunzia: mfano Kitabu cha mwanafunzi mwenyewe.

Kielelezo 9.2 kinaonesha mfano wa jibu la mtahiniwa aliyetoa maana ya zana za kufundishia na kujifunzia badala ya zana za upimaji katika somo la Uraia.

### 2.1.10 Swali la 10


Swali hili lilitoka katika mada ya "Upimaji na Tathmini". Swali hili lilikuwa na vipengele viwili. Katika kipengele (a) mtahiniwa alitakiwa atoe maana ya tathmini, na katika kipengele (b) mtahiniwa alitakiwa aainishe faida tatu za kumtathmini mwanafunzi katika somo la Uraia. Watahiniwa 4991, sawa na asilimia 98.1, walipata ufaulu mzuri wa alama 03 hadi 04. Watahiniwa 35, sawa na asilimia 0.7, walikuwa na ufaulu wa wastani wa alama 02 hadi 2.5 na watahiniwa 60 sawa na asilimia 1.2 walipata alama 00 hadi 1.5 ambao ni ufaulu hafifu. Chati Na. 10 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili kwa asilimia.




**Chati Na. 10:** *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia*

Asilimia 98.1 ya watahiniwa waliofanya vizuri swali hili walionesha kuwa na uelewa wa kutosha katika mada husika, pengine kwa kuwa mada hii hufundishwa katika masomo karibu yote waliyosoma. Watahiniwa hao waliweza kukidhi matakwa ya swali kwa kutoa majibu sahihi kama swali lilivyohitaji. Majibu sahihi ya swali hili yalikuwa kama ifuatavyo: kipengele (a) *Tathmini ni mchakato wa uchunguzi makini, ukusanyaji wa data, uchambuzi wa data na kutafsiri data kwa lengo la kutaka kujua ni kwa kiasi gani mwanafunzi amepata ujuzi uliokusudiwa na kuweza kufanya uamuzi muafaka.* Wakati baadhi ya hoja sahihi kwa kipengle (b) ni kama vile*: Kupata taarifa kuhusu ubora wa njia na vifaa vya kufundishia na kujifunzia, kupata taarifa kuhusu ubora wa majaribio amabyo mwalimu aliwapatia wanafunzi wake* n.k. Kielelezo 10.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili vizuri.

**Kielelezo 10.1**



1. (a) Tathmini ni utaratibu ambao unafanywa na Mwalimu katika kujua uwezo wa Mwanafunzi uko kwa kiwango gani na kuweza kuboresha mbinu za ufundishaji na ujifunzaji.

(b) i/ Humsaidia Mwalimu kuboresha njia/mbinu za kufundishia na kujifunzia

ii/ Humsaidia Mwalimu kujua ni kwakiasi gani Mwanafunzi amepata ujuzi na stadi fulani


iii/ Humsaidia Mwalimu je Mwanafunzi aendelee na ngazi fulani katika elimu.

Kielelezo 10.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kueleza maana ya tathmini na faida za kumtathmini mwanafunzi katika somo la Uraia.

Hata hivyo, asilimia 0.7 ya watahiniwa waliopata alama 02 hadi 2.5, wengi wao walijibu kipengele (a) na kushindwa kujibu kipengele (b) kwa usahihi na hivyo kupata alama za wastani.

Aidha, asilimia 1.2 ya watahiniwa waliopata alama 00 hadi 1.5, baadhi yao walishindwa kubaini matakwa ya swali na wengine walionesha kutokuwa na maarifa katika mada husika. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa maana ya tathmini kama ni *kitendo cha kujua kuwa wanafunzi wameelewa somo? na mwalimu amelithishwa juu ya alichofundisha au la.* Mtahiniwa pia alizidi kuchanganya maana na kuonesha aina za tathmini, ambayo yote hayakuwa majibu sahihi kama inavyoonekana katika kielelezo 10.2.

**Kielelezo 10.2**


10. (a) Tathmini-Ni Kitendo cha Kuchunguza
Kuchambua, kujua kuwa baada
ya Kipindi wanafunzi wamele-
wa somo?, na Mwalimu pia am
elithishwa juu ya alichofundi
sha au la
mfano: wa tathmini zipo mbili
Tathmini ya mwanafunzi
Tathmini ya Mwanafunzi

Kielelezo 10.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kutoa maana sahihi ya tathmini na kushindwa kuanisha faida za kumtathmini mwanafunzi katika somo la Uraia.

## 2.2 SEHEMU B


Sehemu B ilikuwa na maswali matatu (03) ambapo mtahiniwa alitakiwa kuchagua maswali mawili (02) tu. Kila swali lilikuwa na alama kumi na tano (15). Hivyo sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama thelathini (30).

### 2.2.1 Swali la 11

Swali lilitoka katika mada ya "Dola" katika kipengele cha Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Swali lilimtaka mtahiniwa kuchambua shughuli tano za Baraza la Wawakilisha Zanzibar. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 3855, sawa na asilimia 75.8 ya watahiniwa wote 5086. Watahiniwa 1231, sawa na asilimia 24.2%, hawakuchagua kujibu swali hili. Kati ya watahiniwa waliochagua kujibu swali hili, watahiniwa 1855, sawa na asilimia 48.1 walipata ufaulu wa wastani wa alama 06 hadi 10. Watahiniwa 1615, sawa na asilimia 42 walikuwa na ufaulu hafifu wa alama 00 hadi 5.5 na watahiniwa 385 (10%) walipata ufaulu mzuri wa alama 10.5

hadi 15. Chati Na. 11 inaonesha viwango vya ufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.

.




**Chati Na. 11:** *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Baadhi ya watahiniwa waliopata alama kati ya 06 hadi 10 katika swali hili, walishindwa kutoa utangulizi uliojitosheleza na walishindwa kutoa maelezo ya kina kutetea hoja zao. Wengine walirudia hoja, hivyo kupata alama pungufu.

Watahiniwa waliopata alama 00 hadi 5.5 walishindwa kuchambua shughuli tano za Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Wengi wao walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada hiyo na wengine walichanganya maarifa pamoja na uandishi mbaya wa insha uliopelekea kupata alama hafifu. Kwa mfano, mtahiniwa alichanganya maarifa kwa kutoa hoja kama: *uhamiaji kusimamia uhamiaji*, *polisi kusimamia mambo ya ulinzi*, *magereza kusimamia mambo yanayohusu magereza* na *mahakama kusimamia shughuli za mahakama* ambavyo ni vyombo vya ulinzi na usalama na kazi zake. Mtahiniwa mwingine alionesha kazi za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania badala ya kuchambua shughuli za Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Kielelezo 11.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali na hivyo kupata ufaulu hafifu.

**Kielelezo 11.1**

11. Chambua shughuli tano za baraza la wawakilishi la zanzibari

Baraza la wawakilishi la zanzibar ni chombo kilichoundwa kwa ajili ya kusimamia mambo yanayohusu Zanzibar pamoja na visiwa vyake. zifuatazo ni shughuli za baraza la wawakilishi la zanzibar.

Kusimamia uhamiaji; moja wapo ya shughuli

11. inayofanywa na barazala wawakilishi la zanzibar ni kusimamia masuala yote ya uhamiaji wa raia kutoka bara kwenda zanzibar

Polisi; shughuli nyengine inayofanywa na baraza la wawakilishi la zanzibar ni kusimamia mambo yote ya kulinzi.

Magereza; shughuli nyengine inayofanywa na baraza la wawakilishi la zanzibar ni kusimamia mambo yanayohusu magereza

Kusimamia masuala ya kulinzi; shughuli nyengine inayofanyara na baraza la wawakilishi la zanzibar ni kuhakikisha kuna kuna kwa na ulinzi kabla ya kuingia zan-zibar


Mahakama; shughuli nyengine inayofanywa na baraza la wawakilishi la zanzibar ni kusimamia shughuli zote za mahakama ambapo huwa hukumu watu baada ya kukiuka sheria zilizo wekwa na kufanya kinyume, huyo baraza la wawakilishi husimamia mambo ya kimahakama.

Hivyo basi baraza la wawakilishi la Zanzibar linafanya mambo hayo hapo ili kuhakikisha amani inakuwepo na kuepuka kuingi za wahalifu.

Kielelezo 11.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kuchambua shughuli za Baraza la Wawakilishi Zanzibar kama swali lilivyohitaji.

Asilimia 10 ya watahiniwa waliweza kukidhi matakwa ya swali kwa kuchambua shughuli za Baraza la Wawakilishi Zanzibar vizuri. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza shughuli za Baraza la Wawakilishi Zanzibar kama: *Kuishauri serikali ya Mapinduzi*, *kuidhinisha mapato na matumizi ya Serikali ya mapinduzi* na *kupitisha sheria za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar*. Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na uelewa wa kutosha katika mada husika na uelewa mzuri wa matakwa ya swali. Wengi kati yao walianza na utangulizi uliojitosheleza na maelezo sahihi ya kutetea hoja zao. Kielelezo 11.2 kinaonesha sehemu ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu vizuri na kukidhi matakwa ya swali.

**Kielelezo 11.2**



4 Baraza la wawakilishi la Zanzibar.

Utunzi wa sheria za Zanzibar.

Baraza la wawakilishi la Zanzibar moja kati ya shughuli zake ni kutunga sheria ambazo zitatumika Zanzibar.

Kupitisha bajeti ya Zanzibar, Baraza la wawakilishi Zanzibar linashughulikia upitishwaji wa bajeti ya Zanzibar.

Kuchagua wawakilishi watano watakao ingia katika Bunge la Jamhuri ya muungano wa Tanzania, ambapo katika hao wawakilishi watano yatakiwa kuwepo na wanawake wasio-pungua wawili kati ya hao watano.

Kuisisha matumizi ya serikali ya Zanzibar, katika shughuli hii Baraza la wawakilishi huisisha matumizi ya muda mfupi na ya muda mrefu ya serikali ya Zanzibar.

Kushauri Serikali ya Zanzibar. Baraza la wawakilishi huhusika katika kushauri serikali ya Zanzibar na kupendekeza njia mbalimbali ambazo huweza kutumika katika kuendesha shughuli mbalimbal za serikali.


Kwa kuhitimisha naweza nikasema ya kwamba Baraza la wawakilishi Zanzibar hutofautiana na Bunge la Jamhuri ya Tanzania kwa kuwa Bunge hutunga sheria zinazo tumika Tanzania kwa ujumla ila Baraza

Kielelezo 11.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kuchambua shughuli za Baraza la Wawakilisha Zanzibar.

Aidha, asilimia 24.2% ya watahiniwa hawakuchagua kujibu swali hili, pengine kwa sababu walishindwa kutofautisha maarifa ya kazi za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kazi za Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

### 2.2.2 Swali la 12

Swali hili lilitoka katika mada ya "Utamaduni wetu" katika mada ndogo ya "Kazi." Swali lilimtaka mtahiniwa aeleze umuhimu wa kufanya kazi kwa bidii na uadilifu. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 5033 sawa na asilimia 99 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani wa somo la Uraia ambao ni 5086. Swali hili halikujibiwa na watahiniwa 53, sawa na asilimia 01 ya watahiniwa wote. Watahiniwa 4472 sawa na asilimia 88.9 ya watahiniwa waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu mzuri wa alama 10.5 hadi 15. Watahiniwa 551 sawa na asilimia 10.9 walipata alama 06 hadi 10 ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 10 sawa na asilimia 0.2 walikuwa na ufaulu hafifu wa alama 00 hadi 5.5. Chati Na. 12 inaonesha viwango vya ufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 12:** *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia*

Asilimia 88.9 ya watahiniwa waliopata alama kati ya 10.5 hadi 15 walikuwa na uelewa wa kutosha wa mada husika, pengine kwa sababu dhana ya kufanya kazi kwa bidii na uadilifu huzungumzwa kwa mifano katika mazingira yao kuanzia ngazi ya familia hadi ya nchi. Watahiniwa hao pia walidhihirisha kuwa na uelewa wa matakwa ya swali na hivyo kuweza kueleza umuhimu wa kufanya kazi kwa bidii na uadilifu. Majibu sahihi katika swali hili yalikuwa kama vile: *Kumsaidia mtu kupata mahitaji yake ya msingi na ya lazima, ni kipimo cha utu, husaidia kuleta na kukuza maendeleo katika nyanja zote za miasha* na *huondoa umaskini na njaa.*

Kielelezo 12.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kutoa majibu sahihi katika swali hili.

**Kielelezo 12.1**


12. Kufanya Kazi Kwa bidii na Uadilifu: Ni Kitendo cha mtu kujishughulisha kikamilifu Katika shughuli mbalimbali za kimaendeleo kwa jitihada zake zote pasipo kusita. Kufanya Kazi kwa juhudi (bidii) na uadilifu kuna manufaa makubwa kwa mtu na taifa kwa ujumla.

Ufuatao ni umuhimu wa Kufanya Kazi Kwa bidii na maarifa (uadilifu).

Humsaidia mtu kuwa na maendeleo katika maisha: maendeleo ya mtu hayaletwi na kutokukaa tu bila ya kujishughulisha kwa bidii na uadilifu bali yanaletwa na mtu kufanya kazi kwa juhudi (bidii) na uadilifu kupitia kazi anayoifanya na hivyo kufanya aishi maisha mazuri na kumfanya atoke katika hali ya chini aliyokuwepo awali na kuwa katika hali ya juu kwamfano mtu anapofanya kazi kwa bidii anaweza akajenga nyumba akanunua gari na akafungua miradi mbalimbali.

Husaidia kuleta maendeleo ya Taifa: taifa lenye watu wanaofanya kazi kwa juhudi na uadilifu ni taifa ambalo ni rahisi kukuwa kiuchumi na kupiga hatua ya kimaendeleo kutokana na watu wake kufanya kazi kwa bidii na uadilifu mfano katika tanzania wapo watu mbalimbali ambao wanafanya kazi kwa juhudi (bidii) na uadilifu kama vile mohammed dewji ambaye anasaidia katika kuleta maendeleo ya Taifa.

Humsaidia mtu kutatua matatizo yake: mtu anapofanya kazi kwa bidii na uadilifu inamfanya aweze kutatua matatizo yake binafsi ambayo yanamkabili katika maisha yake Kwani huweza kupata fedha zinazomsaidia ka



tika kuyatatua matatizo yake. tofauti na mtu amba
ye hafanyi kazi kwa bidii na uadilifu huweza ku
shindwa kuyatatua matatizo yake binafsi.
Humfanya mtu apandishwe cheo au daraja: uad
ilifu katika kazi unamfanya mtu apandishe cheo
na serikari, kampuni au sehemu yoyote anayofa
nyia kazi kwamfano wanajeshi wanapokwenda
vitani na kufanya kazi yao kwa bidii na uadili
fu wanaporudi nyumbani (makao makuu yao) huw
eza kupandishwa vyeo au madaraja.
Humfanya mtu aaminiwe na watu (jamii): mtu
anapofanya kazi kwa bidii na uadilifu jamii
inayomzunguka itamuamini na kumpenda kuto
kana na jitihada zake anazozionyesha lakini
mtu anapokuwa siyo muadilifu na wala sio anay
efanya kazi kwa bidii jamii haiwezi ikamuami
ni kwa asilimia mia moja kwani inamchukulia
kama mbabaishaji kwamfano mtu anayetenda haki
sawa huweza kuaminiwa na jamii inayomzunguka.
Husaidia kuwa mfano mzuri wa kuig
wa: mtu au nchi inapofanya kazi kwa bidii na
uadilifu inasaidia kuwa mfano mzuri wa
kuigwa na watu au mataifa mbalimbali ku
tokana na utendaji wake wa haki na kukuw
a kimaendeleo zaidi kutoka hatua moja na
nyingine na hivyo mtu au nchi nyingine kupenda
suala hilo na kuweza kuliiga. mfano ni nchi ya Tanzania
chini ya uongozi wa raisi magufuli ni mfano mzuri wa kuigwa.
Kwaujumla ni vyema watu wakafanya
kazi kwa bidii na uadilifu ili waweze kufikia
malengo waliyoyakusudia wayafikie au yaliy
okusudiwa kuyapata na si kukaa tu vijiweni.


Kielelezo 12.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kutoa utangulizi na hitimisho lililojitosheleza. Hata hivyo, mtahiniwa aliweza kuonesha umuhimu wa kufanya kazi kwa bidii na uadilifu kama swali lilivyohitaji.


Asilimia 10.9 ya watahiniwa waliopata alama 06 hadi 10 walishindwa kutoa maelezo sahihi kutetea hoja zao na wengine walitoa hoja pungufu ya

zilizohitajika kwenye swali. Kati yao, wapo walioshindwa kabisa kutoa utangulizi na hitimisho na wengine walikosa maarifa juu ya mpango mzuri wa uandishi wa insha.

Aidha, wapo watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu wa alama 00 hadi 5.5 katika swali hili. Wengi kati yao walitoa maelezo yasiyotetea hoja zao na pia miongoni mwao walishindwa kutoa utangulizi na hitimisho zuri na hivyo kupata alama hafifu. Baadhi yao walitoa hoja chache ambazo hazikuwa na ufafanuzi wa kutosha. Aidha wengine waliandika hoja ambazo hazikuwa na uhusiano na kile kilichoulizwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza umuhimu wa bidii na uadilifu badala ya kueleza umuhimu wa kufanya kazi kwa bidii na uadilifu kama inavyoonekana katika Kielelezo 12.2.

**Kielelezo 12.2**


12 Bidii na Uadilifu, Ni Matendo yanayomfanya
Mtu kuonyesha Maadili Mema kwa Watu wa
ngine na kuweza kuleta Maendeleo kwa ~~baadae~~
baadae Mfano kuwa na heshima Wakati wa
kufanya kazi, kuonyesha Ushirikiano Chany
a kwa jamii inayomzunguka, kuwa Mtiifu
na kuweza kuwa Mvumilivu wa Mambo mba
limbali yanayomkumba katika Shughuli za
kuleta maendeleo katika jamii. Ifuatayo ni
faida za Umuhimu wa bidii na Uadilifu
Humsaidia Mtu kuona kuwa anamaadili
Mema kwa Mfano kukesha kazi anayoifanya


na kuwa na Upendo na jamii inayomzunguka na kuweza kushirikiana nao vizuri

Humsaidia mtu kuwa na Nidhamu inayotakiwa, kama mtu hana bidii na uadilifu hawezi kuwa na nidhamu wakati wa utendaji kazi

Humsaidia mtu kuwa na Ushirikiano mzuri katika kufanyakazi, Mfano mtu kama haonyeshi Ushirikiano wa kufanyakazi anakuwa na kazi nzito ya Uletaji wa maendeleo kwa jamii inayomzunguka.

pia bidii ~~na~~ ~~ma~~ inamsaidia mtu kusifika au kuheshimika, kwa sababu ya Utendaji kazi katika jamii Mfano rais wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh John pombe Magufuli anasifika katika Uchapakazi wake katika jamii na mataifa mengine nje ya Tanzania.

Husaidia kuleta Upendo na Mshikamano mzuri, katika kufanyakazi kwa ~~bad~~ bidii Unaweza kuongeza Upendo na Mshikamano wa kuongeza Maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa Ujumla.


pia kufanyakazi kwa bidii huweza kuleta Uvumilivu na moyo wa kuthaminiwa na jamii kama vile jamii kupendeshwa katika Utendaji kazi kufanyakazi kwa bidii na kwa Uvumilivu wa hali ya juu

Hivyo basi bidii na Uadilifu wa kufanya kazi ni muhimu kwa sababu kuweza kuheshimiwa na pia kuthaminiwa na jamii katika Uvumilivu wako.

Kielelezo 12.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kueleza umuhimu wa kufanya kazi kwa bidii na uadilifu na hivyo kupata alama hafifu.

### 2.2.3 Swali la 13

Swali hili lilitoka kwenye mada ya "Uhusiano wa Kimataifa". Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1213, sawa na asilimia 23.8 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Swali lilimtaka mtahiniwa aeleze misingi mitatu ya sera ya mambo ya nje ya Tanzania na kisha aoneshe namna mwananchi anavyofaidika na sera hiyo. Watahiniwa 3873, sawa na asilimia 76.2 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani hawakuchagua kujibu swali hili. Watahiniwa 495 sawa na asilimia 40.8 walipata ufaulu wa wastani ambao ni kati ya alama 06 hadi 10. Watahiniwa 447 sawa na asilimia 36.9 walipata ufaulu hafifu wa alama 00 hadi 5.5 na watahiniwa 271 sawa na asilimia 22.3 walipata ufaulu mzuri wa alama 10.5 hadi 15 kama inavyoonekana katika Chati Na. 13.





**Chati Na. 13:** *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia*

Baadhi ya watahiniwa waliopata ufaulu wa wastani katika swali hili, waliweza kueleza misingi ya sera ya mambo ya nje ya Tanzania na walishindwa kuonesha kwa usahihi namna mwananchi anavyonufaika na sera hiyo. Wengine walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi na wachache kati yao walirudia hoja na hivyo kupata alama pungufu.

Watahiniwa waliopata alama kati ya 00 hadi 5.5 walishindwa kutambua matakwa ya swali na wengi wao walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha juu ya dhana ya sera ya mambo ya nje ya Tanzania. Wengine walichanganya maarifa na kueleza hoja ambazo hazina uhusiano kabisa na

matakwa ya swali. Kielelezo 13.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyetoa hoja ambazo hazina uhusiano na sera ya mambo ya nje ya Tanzania.

**Kielelezo 13.1**



13. Misingi mitatu ya sera ya mambo ya nje ya Tanzania na katika hoja tatu kuonesha namna ambayo mwananchi anayofaidika na sera hiyo.

Sera ya mambo ya nje; Ni jumla ya mambo yote yanayohusika badhaa katika nje na kuletwa. Ihapa nchini na kuwasaidia wananchi wananufaika nayo. Zifuatazo ni misingi mitatu ya sera ya mambo ya nje ya Tanzania nazo ni;

Misitu ni ~~chab~~ mali; kwamba hao-wazee wanje walikuwa na usemi kwamba misitu ni mali tukitunza, mazingira na kupata miti mengi tunakata na kupanda zingine tunauza na kupata kipato cha juu katika maisha kwamba tukiuza inasaidia kuinua uchumi wa mwananchi mwenye na pia uchumi wa serikali utakuwa wa juu.

13 Chakula ni afya; Hii ni misingi mojawapo
ya mambo ya nje ya Tanzania kwamba
chakula ni afya inasaida watu wakapa
ta mazao kwa ajili ya chakula wanawe
kuwa na Afya njema hata ya kufanya kazi
vizuri ndiyo maana watu wa mambo
ya nje wamesema hilo semo kwamba
tujitahidi katika Shughuli ili tupate
afya na nguvu za kutosha.
Maji ni uhai; Hii misingi ya sera
ya mambo ya nje ya Tanzania kwamba
maji ni uhai katika maisha ya kila
siku tunatakiwa tutunze vyanzo vya maji
ili ya tusaidia katika maisha yetu ya kila
siku kwa sababu tusipotunza mazingira
yetu au vyanzo vya maji inasababisha
tukose maji kwa hiyo tunatakiwa
kutunza vyanzo vya maji ili tupate maji
namna mwananchi anavyofaidika na sera
hiyo kama tuatayo.
Kuongeza kipato chanchi kutokana
uhunzaji wa misitu. Hii namnamna
mwananchi anavyofaidika na sera hiyo
kwamba alipata kipato nyingi cha fedha
kutokana jinsi aliyotunza mazingira
yakamsaidia kupata fedha za kumudu
maisha yao kwa kupata malazi
mavazi, vitu vingine ambavyo alikuwa
akihitaji katika maisha ya kila siku
kwa hiyo tunatakiwa kutunza
mazingira yetu ili tupate faida
nyingi zaidi

Kielelezo 13.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali, kwa kutoa hoja kama chakula ni afya, maji ni uhai ambazo ni kinyume na matakwa ya swali.

Miongoni mwa watahiniwa waliochagua kujibu swali hili, asilimia 22.3 walipata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao walielewa matakwa ya swali na waliweza kueleza misingi ya sera ya mambo ya nje ya Tanzania na kisha kuonesha namna mwananchi anavyofaidika na sera hiyo. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kina katika mada husika, pengine kwa sababu walifundishwa vizuri au walipata maarifa hayo kupitia machapisho mbalimbali na vyombo vya habari. Kielelezo 13.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata ufaulu mzuri katika swali hili.

**Kielelezo 13.2**

13. Sera ya mambo ya nje ya Tanzania ni mipango ambayo huandaliwa kwa ajili ya kushirikiana na nchi za nje katika shughuli za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Kuna sera mbalimbali za nje ya mipaka ya Tanzania kama vile ubinafsishaji, kufuata maendeleo, Uchumi huu unahitaji ushirikiano wa nchi zingine kama vile Kenya, masekoni, Afrika kusini n.k.

Yafuatayo ni misingi ya sera ya mambo ya nje ya Tanzania.

Kudumishe amani na mahusiano katika nchi mbalimbali, ni sera ya mambo ya nje ya Tanzania ambayo husaidia kukua kwa uchumi wa nchi katika kutoa misaada katika taifa la Tanzania. Kutumia na kujadili mbinu mbalimbali za kukuza uchumi wa nchi.

Kudumisha ulinzi na usalama, ambayo ni moja wapo ya mbinu kera inayosaidia kukua kwa uchumi kwa nchi mbalimbali katika Afrika na Ulaya, Ukiangalia katika nchi ambazo kuna ulinzi na usalama zinakuwa kwa haraka ukilinganisha na nchi ambazo kuna migogoro ya kisiasa kama vile Somalia na Demokrasia ya Kongo.

Kuondoa vikwazo katika mipaka ili kusaidia wafanya biashara kufanya biashara kwa uhuru kupitia masoko huria. Kupitia sera hizo zinasaidia kwa kuwepo kwa ukuaji wa kuongezeka kwa miradi mbalimbali kama ujenzi wa miundombinu na barabara.

Yafuatayo ni manufaa ya sera za mambo ya nje ya Tanzania kwa wananchi.

Husaidia wananchi kupata huduma mbalimbali za jamii kama vile, afya, elimu, maji n.k, kupitia

13. Sera za nje ya Tanzania wananchi wamekuwa wakinufaika
na sera hizo kwa kuzingatiwa katika utekelezaji
wa kufikia uchumi wa kati ifikapo 2020.
Kusaidia wananchi kufanya biashara nje ya
mipaka ya Tanzania kama vile Dubai, Kenya, uganda,
Afrika kusini n.k. Kutokana na uhaba wa sukari na
mafuta hapa nchini serikali huomba mafuta na
sukari kutoka katika nje ya mipaka ya nchi.
Huweza kusaidia mwananchi kupata VISA
na kwenda kufanya kazi nje ya nchi, kutokana na
hali hiyo huweza kupata fursa ya ajira katika
nchi za nje kama vile Kenya, Afrika kusini Ghana
hata ulaya.
Sera za mambo ya nje ya Tanzania zimenufaika
nakufwa hasa katika sekta ya ukuaji wa uchumi
wa nchi kupitia shughuli mbalimbali kama vile ya
uchimbaji wa madini kilimo na ufugaji kwenda
vya biashara mbalimbali kama vile sabuni n.k.


Kielelezo 13.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kueleza misingi ya sera ya mambo ya nje ya Tanzania na namna mwananchi anavyonufaika na sera hiyo. Hata hivyo, mtahiniwa hakupata alama zote kutokana na dosari ndogo ndogo katika maelezo yake.

## 2.3 SEHEMU C

Sehemu (C) ilikuwa na maswali matatu (03) ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali mawili (02) tu. Kila swali lilikuwa na alama kumi na tano (15) hivyo, sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama thelathini (30).

### 2.3.1 Swali la 14

Swali hili lilitoka katika mada ya "Misingi ya Ufundishaji wa Somo la Uraia". Swali lilimtaka mtahiniwa kuonesha athari sita za kutofundisha vyema mada ya uchambuzi wa masuala chanya na hasi ya kiserikali na kisiasa. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 2878 sawa na asilimia 56.6 ya watahiniwa wote waliofanya somo hili. Watahiniwa 2065 sawa na asilimia 71.8 walipata ufaulu mzuri wa alama 10.5 hadi 15. Watahiniwa 726, sawa na asilimia 25.2 walipata ufaulu wa wastani wa alama 06 hadi alama 10.5 na watahiniwa 87 sawa na asilimia 3.0 walipata ufaulu hafifu wa alama 00 hadi 5.5 kama inavyoonekana katika Chati Na. 14.




**Chati Na. 14:** *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia*

Watahiniwa waliopata ufaulu mzuri katika swali hili waliweza kuonesha athari za kutofundisha vyema mada ya uchambuzi wa masuala chanya na hasi ya kiseikali na kisiasa. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika na walielewa vema matakwa ya swali. Majibu sahihi katika swali hili yalikuwa kama ifuatavyo: *Wanafunzi kukosa kufikiri kwa kina juu ya maswala chanya na hasi ya serikalini na siasa, wanafunzi kukosa mbinu za kutafuta taarifa za ukweli na uhakika juu ya utendaji wa serikali na mambo ya siasa, kukosekana kwa raia wema na*

*viongozi bora* n.k. Kielelezo 14 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kupata ufaulu mzuri katika swali hili.

**Kielelezo 14**

14. Maswala hasi na maswala chanya ya ~~se~~ kiserikali na kisiasa ni yale mambo yote ya kisiasa ambayo hasa hufanywa na watawala wa serikali. Zifuatazo ni athari za kutofundisha vyema mada ya uchambuzi wa masuala chanya na hasi ya kiserikali na kisiasa.

Kuchagua viongozi wasiofaa. Hali hii hutokea kwa wanafunzi kutokufahamu masuala chanya na hasi ya kiserikali na kisiasa na hatimaye kuchagua viongozi shuleni au kwenye jamii yao.

14 wasifae kuigwa. Kwa kutosikiliza matatizo ya watu wanaowaongoza.

Kuwepo kwa unyanyasaji katika uongozi. Viongozi kuweza kutoa viongozi wengine au kuingilia kazi ya kiongozi mwingine madarakani bila maelewano hivyo huweza kuwajengea wanafunzi kuwepo kwa unyanyasaji wawapo shuleni katika uongozi wao.

Kutokuwepo kwa haki za kibinadamu. Mwalimu kutofundisha mada hii ya masuala hasi na chanya ya kiserikali na kisiasa mwanafunzi hatafahamu haki anazostahili kupata kutoka katika jamii kwa ujumla.

Mwanafunzi kutofahamu shughuli mbalimbali zinazofanyika serikalini. Kwa sababu baadhi ya viongozi kutokuwa waaminifu katika uongozi wao na baadhi kuwa waaminifu. Mfano. Kutoa rushwa kwa wananchi ili waendelee kuchaguliwa.

Kuwepo kwa rushwa. Hii hutokea kwa wanafunzi kutofahamu kama ni suala chanya au hasi kuhusu uongozi na kuendeleza katika uongozi wa shule, kati ya kiongozi wa shule na mwanafunzi ambaye siyo kiongozi.

Kuwepo kwa muingiliano wa madaraka. Hii hutokea viongozi kwa wanafunzi kutofahamu maswala hasi na chanya hivyo na hivyo kuingiliana kimadaraka bila kuwepo na makubaliano yoyote hivyo na kutoelewana.

Hivyo basi; mwalimu anashauriwa kuchambua mada ya kufundisha vyema mada


Kilelezo 14 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyekidhi matakwa ya swali kwa kuonesha athari za kutofundisha vyema mada ya uchambuzi wa masuala chanya na hasi ya kiserikali na kisiasa.

Asilimia 25.2 ya watahiniwa walitoa hoja pungufu pamoja na maelezo yasiyokuwa na mifano. Pia baadhi yao walishindwa kutoa utangulizi mzuri na hitimisho zuri na hivyo kupata alama za wastani. Wengine walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi katika insha zao.

Aidha, asilimia ndogo ya wathiniwa (3.0%) waliopata alama hafifu walishindwa kuonesha kwa usahihi athari za kutofundishwa vyema mada ya uchambuzi wa masuala chanya na hasi ya kiserikali na kisiasa. Baadhi yao walishindwa kutoa utangulizi uliojitosheleza, maelezo ya kina kutetea hoja zao na hitimisho lenye uhusiano na hoja. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama vile: *huchochea ukoloni mamboleo, matabaka* na *ubaguzi wa kijinsia katika uongozi* ambazo hazikuwa na maelezo yenye kujitosheleza na hivyo kupata alama hafifu.

### 2.3.2 Swali 1a 15

Swali hili lilitoka katika mada ya "Uchambuzi wa Machapisho/Maandiko Muhimu ya Kufundishia na Kujifunzia Somo la Uraia". Swali lilimtaka mtahiniwa achambue mbinu sita zinazoweza kutumika katika kukusanya machapisho bora ya ziada ya somo la Uraia. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 2212, sawa na asilimia 43.4 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Watahiniwa 1291, sawa na asilimia 58.4 walipata ufaulu hafifu wa alama 00 hadi 5.5. Watahiniwa 688 sawa na aslimia 31.1 walikuwa na ufaulu wa wastani wa alama 06 hadi 10 na watahiniwa 233 sawa na asilimia 10.5 walipata ufaulu mzuri wa alama 10.5 hadi 15 kama inavyoonekana katika Chati Na. 15.





**Chati Na. 15:** *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia*

Watahiniwa waliopata alama 00 hadi 5.5, walishindwa kukidhi matakwa ya swali na wengine walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika. Aidha, wapo waliochanganya maarifa kwa kuchambua mbinu za kufundishia na kujifunzia badala ya mbinu za kukusanyia machapisho ya ziada ya somo la Uraia. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama: *Kazi mradi*, *uwasilishaji*, *mbinu ya majadiliaano*, *mbinu ya maswali na majibu*, *onesho mbinu* na *mbinu ya ziara* kama inavyoonekana katika Kielelezo 15.1.

**Kielelezo 15.1**

15 Machapisho ya ziada; Hayo
ni Maandiko ambayo Mwalimu
na Mwanafunzi husoma ili kuyaong
ezea Maarifa;
Zifuatazo ni mbinu zinazoweza
kutumika katika kukusanya Machapi
sho bora ya ziada ya Somo la Uraia
Kazi mradi; Hii ni mbinu ambayo
inaweza kutumika katika kukusanya
Machapisho bora ya ziada ya somo
la Uraia. Mwalimu Unatoa kazi
mbalimbali za kufanya ili nao
waweze kuleta Majibu
Uwasilishwaji wa kazi za Wiki
ndi. Hii ni mbinu Mojawapo ina
yoweza kutumika katika kukusanya
Machapisho bora ya ziada ya
Somo la Uraia. Wale wanaoyo wa
sikisha husaidia katika kupata Ma
pashu ~~Map~~ Machapisho bora ya
ziada ya Somo la Uraia.
Mbinu ya Majadiliano. Hii
ni mbinu inayoweza kusaidia
katika kukusanya Machapisho
bora ya ziada. Mbinu hii ni muhi
mu husaidia wote kuyaongezea
Maarifa.
Mbinu ya Maswali na Maji
bu. Hii ni mbinu Mojawapo inayo
weza kutumika katika kukusanya
Machapisho bora ya ziada. Mbinu
hii ni Muhimu kwasababu huku


15 Uwezo wa kufikiri.
Mbinu ya Maonyesho au
Onyesho mbinu. Hii ni mbinu
Mojawapo katika kukusanya mach
apisho bora ya ziada. Mbinu hii
humsaidia tuwe na ule Uwezo
wa kukumbuka / Kumbukumbu
ya kitu alichokiona.
Mbinu ya Ziara - Hii ni mbinu
Mojawapo inayoweza kutumika
katika kukusanya machapisho ya
ziada. Mbinu hii ni muhimu
kwa sababu humsaidia mtu kujifu
nza kwa kusikia na kuona pia.
Hivyo huinua kiwango cha uelewa
na kupata ~~Maarifa~~ Maarifa
mbalimbali.
Hivyo basi mbinu hizo ni
muhimu sana kwa sababu humu
ongezea mtu Maarifa na ule Uwe
zo wa kufikiri na kumjengea
kumbukumbu

Kielelezo 15.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyechambua mbinu za kufundishia na kujifunzia badala ya mbinu zinazoweza kutumika kukusanya machapisho bora ya ziada ya somo la Uraia na hivyo kupata alama hafifu.


Aidha, watahiniwa 31.1% waliofanya swali hili walipata alama za wastani kwa sababu baadhi yao walishindwa kufafanua hoja kwa usahihi na wengine walitoa maelezo ambayo hayakujitosheleza katika kutetea hoja zao. Aidha, wapo walioshindwa kutoa maelezo sahihi katika sehemu ya utangulizi na hitimisho na hivyo kupata alama pungufu.

Kwa upande mwingine, watahiniwa wachache (10.5%) waliopata alama 10.5 hadi 15 waliweza kuchambua mbinu zinazoweza kutumika katika kukusanya machapisho bora ya ziada ya somo la Uraia. Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika na waliweza kutambua matakwa ya swali. Baadhi ya majibu sahihi katika swali hili

yalikuwa kama ifuatavyo: kutambua vyanzo vyote vya machapisho ya ziada kama vile *maktaba*, *kuchambua aina za machapisho ya ziada kama vile magazeti n.k*, *kuzingatia gharama kama vile magazeti*, *majarida na vitabu n.k.* Kielelezo15.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

**Kielelezo15.2**

15. Machapisho ya ziada ni makala mbali-
mbali ambazo zina nukuu za somo ambazo huwe-
za kurahisisha kupata maarifa, stadi na mwelekeo wa
kufundisha na kujifunza somo fulani. Machapisho ya
ziada ni kama vile vitabu, magazeti, majarida na
makala mbalimbali. Mbinu zinazoweza kutumika
katika kukusanya machapisho ya ziada ya somo
la uraia, ni pamoja na hizi zifuatazo;-
Kuhudhuria semina na makongamano,
yanayohusu somo la uraia, mwalimu anapaswa kuh
udhuria semina na makongamano mbalimbali ili-
aweze kupata machapisho ya ziada ya kufundishi
a somo la Uraia. Mfano semina hupenda kutoa
majarida mbalimbali kwa watu waliohudhuria
semina hiyo. Mfano semina zinazohusu haki na
wajibu wa binadamu na raia ni moja ya njia
ya kupata machapisho ya ziada ya haki na
wajibu wa binadamu na raia iliyopo kwenye
somo la Uraia.
Kudhuru maktaba, pia kutembelea-
maktaba mbalimbali huweza kumsaidia mtu kukus
anya maandiko ya ziada ya somo la uraia
kwa kuchukua kitabu chenye maudhui mazuri-
ya somo la Uraia na kukichapa ili kuweza
kuondoka na nukuu za somo la uraia. Mfano
mwalimu anaweza kutoa nakala za vitabu vya
somo la uraia kama ni vichache ili kuweza
kupata machapisho ya ziada ya kutosha.
Kuchapisha na kutoa nakala zinazo-
husu somo la uraia ili kuweza kupata maari-
fa zaidi. Hii inatokea pale vitabu vipo vichache
vya somo la uraia, kwa hiyo hutolewa



15 ili kuweza kupata machapisho mengi na-
yatakayokidhi mahitaji ya wanafunzi.
Kununua machapisho, endapo kuna
duka la vitabu lenye vitabu na machapisho mengine
ya somo la uraia ambayo yana maudhui mazuri
na yanayohitajika yanaweza kununuliwa na-
kutunzwa shuleni ili pale yatakapohitajika ya-
patikane kwa urahisi.
Ziara mafunzo, pia inaweza kusaidia
kupata machapisho ya ziada kutokana na ziara
itakayofanyika. Labda ziara hiyo inaweza kuwa
karibu na duka la vitabu au kukatolewa machapish
o ya ziada katika eneo la ziara na kumfa
nya mwalimu pamoja na mwanafunzi kupata
machapisho ya somo la uraia.
Utafiti na majaribio, pia inaweza
kuwa mbinu bora ya kupata machapisho bora
ya ziada kutokana na tafiti zinazofanyika kwa
sababu kuna ripoti ya utafiti na pia majaribio-
yanaweza kusaidia kupata machapisho hayo-
kwa kutoa maswali yatakayofanyiwa uchunguzi
zaidi na kuchapishwa pamoja na majibu yake.
Machapisho ya ziada yanafaida
kwa watumiaji kama vile kupata taarifa muhi
mu na kusoma mada za somo kwa undani
zaidi, kujua mambo kwa kina na kupata
madhana mbalimbali.

Kielelezo 15.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa ambaye alielewa matakwa ya swali na kujibu vizuri swali hili. Hata hivyo mtahiniwa hakuweza kupata alama zote 15 kutokana na kutojitosheleza kwa baadhi ya ufafanuzi katika hoja zake.

### 2.3.3 Swali la 16

Swali lilitoka katika mada ya "Zana za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Uraia". Swali lilimtaka mtahiniwa katika hoja sita, kueleza umuhimu wa mwalimu wa somo la Uraia kufanya majaribio ya zana za kufundshia na kujifunzia kabla ya kuzitumia. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 5041,

sawa na asilimia 99.1 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Watahiniwa 4017, sawa na asilimia 79.7 walipata ufaulu mzuri wa alama 10.5 hadi 15. Watahiniwa 964, sawa na asilimia 19.1 walikuwa na ufaulu wa wastani wa alama 06 hadi 10 na watahiniwa 60 sawa na asilimia 1.2 walikuwa na ufaulu hafifu wa alama 00 hadi 5.5. Chati Na. 16 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 16:** *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia*

Watahiniwa (79.7%) waliojibu swali hili walipata ufaulu mzuri kwani walikidhi matakwa ya swali. Watahiniwa hao waliopata alama za juu waliweza kueleza umuhimu wa mwalimu wa somo la Uraia kufanya majaribio ya zana za kufundishia na kujifunzia kabla ya kuzitumia. Ufaulu huo mzuri katika swali hili pengine ni kwa sababu mada ya zana inafundishwa karibu katika masomo yote wanayojifunza na ilidhihirisha uwezo wao katika kuhawilisha maarifa waliyoyapata katika mafunzo kwa vitendo (BTP). Baadhi ya majibu sahihi katika swali hili yalikuwa kama ifuatavyo: *Kuona kama zana hiyo ni nzima au mbovu, humsaidia mwalimu kujiamini katika ufundishaji wake, kufamu madhara yanayoweza kuletwa na zana hiyo* n.k. Kielelezo 16.1 ni sehemu ya sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri.

**Kielelezo 16.1**

16. Majaribisho ya zana za kufundishia ya kujifunzi ni jumula ya vitendo ambavyo mwalimu huvifanya ili kubaini au kugundua kama zana za kufundishia na kujifunza zina ubora au mapungufu pia kama zinaweza kufikisha lengo mahususi kwa walengwa.

Ufuatao ni umuhimu kwa mwalimu wakati wa kufanya majaribio ya zana za kufundishia na kujifunzia kabla ya kuzitumia katika somo la Uraia.

Humsaidia mwalimu kujua ubora na mapungufu ya zana hiyo ili kuweza kufanya marekebisho na maboresho zaidi hivyo huweza kutumia zana kwa usahihi na kufikia malengo aliyoyakusudia.

Humsaidia mwalimu wa somo la Uraia kugundua kama zana inaendana na mada inayofundishwa kwani pasipo kujaribisha zana huweza kufundisha vitu ambavyo haviendani na zana iliyoandaliwa hivyo basi ni vyema sana kujaribisha zana kabla ya kuitumia.

Humsaidia mwalimu kama zana ina usalama kwa sababu kuna zana zingine zinaweza kusababisha ajali kwa wanafunzi wakati wa kujifunza hivyo basi ni vizuri na ni muhimu kwa mwalimu wa Uraia kufanya majaribio ya zana ili kuepusha ajali wakati wa kufundisha na kujifunzia somo la uraia.

Humsaidia mwalimu kujua kama zana inamjengea udadisi mwanafunzi wakati wa kujaribisha zana za kufundishia na kujifunzia somo la uraia ni muhimu kwa mwalimu kuangalia na kugundua au kubaini kama zana hiyo inajenga udadisi kwa wanafunzi, zana inatakiwa isitoe majibu ya moja kwa moja.

Kielelezo 16.1 ni sehemu ya sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kueleza umuhimu wa mwalimu wa somo la Uraia kufanya majaribio ya zana za kufundishia na kujifunzia kabla ya kuzitumia.

Aidha, asilimia 19.1 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani, ambapo baadhi walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Wengine walishindwa kutoa utangulizi na hitimisho lisilojitosheleza na hivyo kupata alama pungufu.

Hata hivyo, asilimia 1.2 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu. Uchambuzi ulionesha kuwa baadhi yao hawakuelewa matakwa ya swali na wengine walitoa hoja pungufu bila ya kuwa na maelezo yenye mifano kutia nguvu hoja zao. Kwa mfano, mtahiniwa alitaja hoja tano bila kutoa maelezo kama alivyotakiwa pamoja na kushindwa kabisa kutoa utangulizi na hitimisho na hivyo, kupata alama hafifu. Kielelezo 16.2 kinaonesha mtahiniwa aliyeshindwa kutoa majibu yake katika insha kama swali lilivyohitaji na hivyo, kupata ufaulu hafifu.

**Kielelezo 16.2**

16. (i) Ili kuzingatia usalama wa walengwa ili zizijo kuwadhuru wanafunzi na yeye mwenyewe.

(ii) Ili kuhakikisha kwamba hazina ubaguzi wa kijinsia

(iii) Ili kuhakikisha kama zitaendana na mada husika anayofundisha.

(iv) Ili kuhakikisha ubora wake na ukubwa ili zionekane na walengwa wote

(v) Ili kuhakikisha kama zina mjengea mwanafunzi uelewa na udadisi

Kielelezo 16.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali. Mtahiniwa hakuwa na maarifa ya kutosha ya uandishi wa insha na hivyo kushindwa kupata alama za juu.

## 3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU CHA WATAHINIWA KWA KILA MADA

Kiwango cha ufaulu katika mada zilizotahiniwa mwaka 2018 kilikuwa kizuri kwani asilimia **86.2** ya watahiniwa walipata wastani wa alama 40 na zaidi.

Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika mada za mtihani wa 612 Uraia kilionesha kuwa watahiniwa walifanya vizuri katika mada karibu zote hasa katika mada ya *Utamaduni Wetu* ambapo ufaulu ulikuwa asilimia 99.4; *Zana za kufundishia na kujifunzia*, asilimia 98.8; *Maandalizi ya Kufundisha Somo la Uraia,* asilimia 98.7; *Upimaji na Tathmini,* asilimia 98.1; *Uchumi wa Tanzania,* asilimia 89.5; *Misingi ya Ufundishaji wa Somo la Uraia,* asilimia 79.7; *Dola,* asilimia 78.7; na *Uchambuzi wa Maandiko/Machapisho muhimu ya kufundishia na kujifunzia somo la Uraia,* asilimia 70.3. Aidha, mada ya *Uhusiano wa Kimataifa* ilikuwa na ufaulu wa wastani wa asilimia 63.1. Hakukuwa na mada iliyokuwa na ufaulu hafifu katika somo hili. (Tazama **Kiambatisho**)

Ufaulu mzuri wa mada katika somo hili ulionesha kuwa watahiniwa walifanya vizuri karibu katika mada zote kwa mwaka 2018 kutokana na watahiniwa wengi kuwa na ujuzi na weledi wa kutosha kuhusu mada mbalimbali zilizotahiniwa.

## 4.0 HITIMISHO

Kwa ujumla, mtihani wa somo la Uraia wa 2018 ulizingatia muhtasari wa somo la Uraia na ulizingatia majazi yote ya utambuzi kama vile maarifa, ufahamu, matumizi, uchambuzi, uundaji na tathmini. Kwa ujumla, kiwango cha ufaulu kwa mwaka 2018 kilikuwa kizuri kwa kuwa wastani wa kiwango hicho katika mada zote ulikuwa ni asilimia **99.98**.

Uchambuzi uliofanyika unaonesha changamoto mbalimbali za watahiniwa wachache walioshindwa kupata alama za juu kama vile uelewa mdogo wa matakwa ya swali, uwezo mdogo wa kujibu maswali, kushindwa kuhawilisha maarifa, kutofuata maelekezo na kushindwa kutoa ufafanuzi wa dhana walizoulizwa kwa usahihi na kukosa maarifa ya kutosha kuhusiana na dhana zilizoulizwa.

Taarifa hii itasaidia kuinua kiwango cha ufaulu katika somo la Uraia kwani itatoa msingi kwa wakufunzi na wawezeshaji katika ufundishaji wa mada zilizoonekana kuwa na matatizo. Aidha, taarifa hii itatoa chachu kwa wanachuo na kuwahamasisha katika ujifunzaji wa mada zote za Taaluma na Utaalamu (ufundishaji) zilizopo katika muhtasari wa somo la Uraia.

Mwisho, taarifa hii ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa iwe msingi katika kuwasaidia wakufunzi na wanachuo kuyaelewa makosa yanayosababisha watahiniwa wachache kutojibu vizuri maswali na kisha kurekebisha kasoro zilizojitokeza. Aidha, taarifa hii itakuwa na tija kwa wakufunzi katika ufundishaji, utungaji na usahihishaji wa mitihani yote na hasa ile ya kitaifa na pia itasaidia kuinua kiwango cha kufaulu katika somo hili.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuinua kiwango cha ufaulu kwa wanachuo inapendekezwa kuwa:

(a) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa Elimu, waandae warsha na semina mbalimbali zinazohusiana na somo la Uraia ili kuwapa fursa wakufunzi kujifunza na kuongeza ujuzi katika ufundishaji wa somo hili.

(b) Motisha kwa wakufunzi zitolewe ili kuwahamasisha na kuwajengea ari na uwezo wa kufanya tafiti na kuandika machapisho na makala mbalimbli za somo la Uraia ili kuongeza maarifa na uwezo kwa wakufunzi na walimu wanafunzi katika kujifunza somo hili.

(c) Wakufunzi wa somo hili wanapaswa kufundisha mada zote za taaluma na utaalamu kwa kina na ufasaha ili wanachuo waweze kuonesha umahiri wa somo na kutoa hoja za mantiki kuhusiana na maswali yanayoweza kuulizwa.

(d) Walimu wanafunzi wahamasishwe kujisomea makala na machapisho mbalimbali yanayohusu mada za somo la Uraia na masuala mtambuka ili kuwajengea uwezo na kuamsha ari ya kufanya tafiti ndogondogo za kielimu (action reseaarch).

(e) Wakufunzi wa somo wajenge tabia ya kutoa mazoezi, majaribio na mitihani ya mara kwa mara ikiwa ni ya ujirani mwema au kikanda ili

walimu wanafunzi wapate uzoefu wa namna tofauti za kuulizwa na kujibu maswali.

**Kiambatisho**

## UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA

| Na. | Mada | Namba ya Swali | Asilimia ya Ufaulu | | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Waliopata asilimia 40 na zaidi | Wastani | |
| **1** | Utamaduni Wetu | 4 | 99 | 99.4 | Vizuri |
| | | 12 | 99.8 | | |
| 2 | Zana za Kufundishia na Kujifunzia | 5 | 98.8 | 98.8 | Vizuri |
| | | 16 | 98.8 | | |
| 3 | Maandalizi ya kufundisha somo la Uraia | 7 | 98.7 | 98.7 | Vizuri |
| 4 | Upimaji na Tathmini | 9 | 97.4 | 98.1 | Vizuri |
| | | 10 | 98.8 | | |
| 5 | Uchumi wa Tanzania | 6 | 89.5 | 89.5 | Vizuri |
| 6 | Misingi ya Ufundishaji wa somo la Uraia | 2 | 58.1 | 79.7 | Vizuri |
| | | 8 | 84.1 | | |
| | | 14 | 97 | | |
| 7 | Dola | 1 | 99.3 | 78.7 | Vizuri |
| | | 11 | 58.1 | | |
| 8 | Uchambuzi wa Maandiko/Machapisho muhimu ya kufundishia na kujifunzia somo la Uraia | 3 | 99 | 70.3 | Vizuri |
| | | 15 | 41.6 | | |
| 9 | Uhusiano wa Kimataifa | 13 | 63.1 | 63.1 | Wastani |